



# Habari za msingi kuhusu Ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19)



## Jinsi virusi vinavyoenea kutoka kwa mtu hadi mtu

Watu hupata ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19) kutoka kwa wengine ambao wana virusi hivyo. Ugonjwa huenezwa kuitia matone madogo yanayotengenezwa wakati watu walioambukizwa wanakoho, wanapiga chafya, au wanapumua.

Matone haya yanaweza kuvutwa na watu walio karibu wakati wa kupumua au yanaweza kutua juu ya sura ya vitu vilivyo karibu. Wakati watu wanapumua na kuvuta pumzi yenye matone au kugusa nyuso za vitu vilivyo na matone haya, kisha kugusa macho yao, pua, au mdomo, wanaweza kuambukizwa. Hii ndio sababu ni muhimu kukaa umbali wa zaidi ya mita 1 kutoka kwa mtu mganjwa. Nchi nyingi zimetunga sera za kukaa mbali kati ya mtu na mtu ambazo zinasema kwamba, kwa ulinzi kamili dhidi ya kuenea kwa virusi vya ugonjwa wa corona (COVID-19), watu wanapaswa kukaa angalau umbali wa mita 1 kutoka kwa watu wengine wote isipokuwa familia zao.



## Dalili za maambukizi

Dalili za kawaida za ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19) ni homa, uchovu, na kikohozi kavu. Kwa kawaida, dalili huanza pole pole. Baadhi ya watu wengine walioambukizwa hawaonyeshi dalili na hawajisikii kuumwa. Watu wengi (karibu 80%) hupona bila matibabu maalum. Karibu mtu 1 kati ya watu 6 huwa mganjwa sana. Wazee na watu wenye matatizo ya kiafya kama vile matatizo ya moyo, ugonjwa wa kisukari na shinikizo la damu wana uwezekano mkubwa wa kuwa wagonjwa sana. Watu wenye homa, kikohozi, na shida ya kupumua wanapaswa kutafuta matibabu.